JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU

**Kumb.Na HA.54/101/01/46** **19 Desemba, 2025.**

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu anawatangazia Watu wote wenye sifa ya kuwa Mwenyekiti waweze kuomba ili kujaza nafasi hii

### A. SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu
3. Awe ni Mstaafu wa hiyari au kwa laazima katika utumishi wa umma
4. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote
5. Awe na Elimu ya Form IV au VI
6. Awe na taaluma ya kuanzia Astashahada na kuendelea, katika fani yoyote

### B. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

1. Kuendesha/kuongoza vikao vyote vya Kisheria vya Bodi ya ajira

### c. MUDA WA NAFASI HIYO

Muda wa nafasi ni Miaka Mitano (5)

### D. POSHO

Kazi hii haina Mshahara, Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na Vikao vitakavyokaliwa na Bodi.

### E. MASHARTI YA JUMLA

1. Muombaji aambatanishe wasifu wake kwenye barua yake ya maombi.
2. Muombaji aambatanishe nakala halisi ya vyeti vyake vya Elimu na Taaluma.
3. Kila muombaji ambatanishe maombi yake na Picha moja (1) za *passiport Size.*

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuanzia 19 Desemba 2025 ya Tangazo hili hadi Tarehe 8 Januari 2026 Saa 9:30 Alasili.

Maombi yatapokelewa kwa njia ya sanduku la Posta au kwa kuwasilishwa katika Masijala ya Ofisi ya Mkurugenzi kwanjia ya Mkono

Anuani ya kutuma maombi ni:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 1288
KISHAPU.

D. S. Mashauri,
Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W),
**KISHAPU.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA KISHAPU
S.L.P 1288 KISHAPU